**MTIHANI WA KIDATO CHA NNE, 2023**
**ELIMU YA DINI YA KIISLAMU (E.D.K.)**
**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**

**SEHEMU A (ALAMA 20)**

| QN | I | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x | xi | xii | xiii | xiv | Xv |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ANS | C | B | E | A | C | B | D | B | E | C | B | A | C | B | B |

**Alama = 15,@ 1**

2.

| **Orodha A** | i | ii | iii | iv | V |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | I | G | B | E | D |

**Alama =5, @ 1**

**SEHEMU B (ALAMA 35)**

3. a) Funga kilugha ni kujizuilia kufanya jambo lolote la kawaida na funga kisheria ni kujizuilia kula, kunywa, kujamiiana na kuingiza kitu chochote katika matundu ya mwili na kumuasi Allah kuanzia alfajiri ya kweli mpaka kuingia magharibi. **(Alama 2)**

b) Nguzo za funga ni
- i) Nia **Alama 1 = @ 0 ½**
- ii) Kujizuilia na kila chenye kufunguza kuanzia alfajiri ya kweli hadi magharibi.

c) Sunna zinazoambatana na funga ya Ramadhani.ni:-
- i) Kuchelewa kula daku
- ii) Kuwahi kufturu
- iii) Kuzidisha kusoma Qur-an **Alama 2 = @ 0 ½**
- iv) Kukaa itikaf
- v) Kutafuta usiku wa laylatul - qadri.

4. a) Dini ni imani ya kuwepo Mungu muumba na mtazamo wa uislamu ni mfumo kamili wa maisha ya mwadamu ya kila siku (**Alama 2)**

b)
- i) Dini ya Mwenyezi Mungu
- ii)Dini za watu **(Alama 1 )= @ 0 ½**

c)
- i) Shirki katika dhati ya Mwenyezi Mungu
- ii) Shirki katika sifa za Mwenyezi Mungu
- iii) Shirki katika mamlaka ya Mwenyezi Mungu
- iv) Shirki katika hukumu za Mwenyezi Mungu **Alama 2 = @0 ½**

5. a)
- i) Zakat na sadaqa
- ii) Jizya
- iii) Alkharaj
- iv) Alghaniima(ngawira)
- v) Alfay -i

vi) Ushru **Alama 2 = @ 0 ½**
vii) Zaraib

b) i) Kusoma suratul fa-tha
ii) Kurukuu **Alama 2 = @ 01**

c) Abubakar **(Alama 1)**

6. a) i) Qur-an ni mashairi aliyoyatunga mtume
ii) Njozi zilizovurugika
iii)Zao la mwenye kifafa
iv)Aya za shetani
v) Uandishi wa Muhamad kwa msaada wa Mayahudi na wa wakristo
vi)Utunziwa Muhamad ili arekebishe tabia za waarabu
vii)Utunzi wa Muhamad ili ajinufaishe kiuchumi **Alama 2 = @ 0 ½**

b) i) Kutojua kusoma kwa Muhamad na kuandika
ii)Qur-an yenyewe inajieleza kuwa ni kitabu cha Allah (s.w)
iii)Hali aliyokuwa nayo mtume katika kupokea wahyi
iv)Qur-an kushushwa kidodo kidogo kwa kipindi cha miaka ishirini na tatu (23)
v) Kukosolewa kwamtume katika Qur-an
vi)Kutokea kweli yake yaliyotabiriwa katika Qur –an
vii)Mpangilio wa Qur-an
viii) Maudhui ya Qur-an na mvuto wa ujumbe wake **Alama 3 @ = 0 ½**

7. a) Sunna ni mwenendo au tabia au mila aliyokuwa akifuata Mtume Muhamad katika maisha yake ya kilasiku. **Alama 1**

b) i) Hadith Nabawiy
ii) Hadith Qudusiy **Alama 1 @ = 0 ½**

c) i) Sanad (Isnad)
ii) Matini
iii) Rawi **Alama 3 = @ 1**

8. a) i) Talaka Khul-u ni aina ya talaka ambayo inapatikana kwa mwanamke kudai aachwe kwa sababu zake mwenyewe .
ii)Talaka zihaar ni aina ya talaka ambayo hupatikana kwa kumsusa mke kwa kumuambia “Nakuona kama mgongo wa mama yangu”.
iii)Talaka Liaan – ni aina ya talaka ambayo hupatikana kwa viapo viwili vya mume na mke ikitokea kwamba mume au mke amemkamata mwenzie ugoni lakini hapana mashahidi wanne walioshuhudia kitendo hicho. **Alama tatu (3) = @ 1**

b) Eda ya kufiwa ni miezi minne na siku kumi na Eda ya kuachwa ni miezi mitatu au twahara tatu . **Alama 2**

9.a) i) Hawali wala kunywa
ii) Wameumbwa kwa Nuru
iii) Hawana matamanio
iv) Hufanya waliyoamrishwa tu **Alama 2 = @ 0 ½**

b) i) Kupeleka wahyi

ii) Kutoa roho
iii) Kupuliza parapanda
iv) Kuandika mema na maovu ya waja
v) Kuwaadhibu wenye kuchupa mipaka
vi)Kuwasaidia waumini katika kupambana na maadui **Alama 3 = @ 0 ½**

## SEHEMU C (ALAMA 45)

10. Zinaa ni kitendo kichafu ambacho humkasirisha Mwenyezi Mungu na kufanywa kati ya mwanaume na mwanamke wasiooana. Yafuatayo ni baadhi ya madhara ya zinaa.
    - Uzinzi unamuweka mtu katika hatari kubwa ya kupata na kueneza maradhi ya uasherati kwani maradhi hayo yataidhoofisha sana afya yake na wengine.
    - Humfanya mtu kutokuwa na aibu, kukosa uaminifu kutawaliwa na fikri za uasherati, utovu wa nidhamu, ulaghai, uongo na ubinafsi na kupupia machafu.
    - Zinaa inasababisha kundi kubwa la vijana katika jamii kufanya ukahaba.
    - Kuruhusu zinaa kutaondosha umuhimu na heshima ya ndoa na hatimaye zinaa itachukua nafasi ya ndoa.
    - Zinaa hutokomeza umma wa binadamu katika malezi hakuna mwanaume atakayekubali kubeba mzigo wa malezi ya mtoto atakayezaliwa.
    - Zinaa italeta watoto wa nje ya ndoa.
    - Zinaa huondoa maelewano katika jamii
        - Utangulizi = 1 ½
        - Hoja 6 = @ 2 = 12
        - Hitimisho = 1 ½
        - Jumla alama 15

11. Kuamini siku ya mwisho ni nguzo ya tano katika nguzo za imani ya kiislamu. Ambayo ndo hupatikana baada ya viumbe kufufuliwa na kusimamishwa mbele ya Allah. Zifuatazo ni sababu zinazolazimu uwepo wa siku ya mwisho.
    - Neema na vipaji alivyotunukiwa mwanadamu ni hoja ya kuwepo siku ya malipo.
    - Kutofautiana vipaji vya mwanadamu ni hoja ya kuwepo siku ya malipo
    - Kuwepo kwa nadharia nyingi za maisha hapa ulimwenguni ni hoja ya kuwepo siku ya malipo ili ibainike njia sahihi.
    - Hapana budi kuwepo siku ya malipo iliwalipwe wale waliotenda mema bila ya ujira hapa ulimwenguni.
    - Hapana budi kuwepo siku ya malipo ili waovu wapate adhabu iliyostahili ya makosa yao.
    - Hapana budi kuwepo siku ya malipo ili waliodhulumiwa walipwe haki zao.
    - Utangulizi = 1 ½
    - Hoja 6 = @ 2 = 12
    - Hitimisho = 1 ½ **<u>Jumla Alama 15</u>**

12.

| SURA ZA MAKKA | SURA ZA MADINA |
|---|---|
| **1. Walengwa.**<br><br>Zilishushwa katika kipindi cha mwanzo wa utume. Hivyo zilizingatia mazingira ya jamii zilizozama kwenye ushirikina. | **<u>1. Walengwa.</u>**<br><br>Zilishushwa katika kipindi ambacho mtume (s.a.w) ameanzisha Dola ya kiislamu. Hivyo sura hizo zililenga waumini |

| | |
|---|---|
| **2. Ujumbe**<br><br>Katika kipindi makka ujumbe wa Qur-an uliwalenga kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa Imani ya kweli juu ya Mwenyezi Mungu, Malaika, vitabu, mitume na siku ya mwisho.<br><br>**3. Muundo**<br><br>Takriban sura zote za makka zina aya fupifupi zenye kufikia lengo moja na pia vilevile nyingi ya sura hizi ni fupi.<br><br>**4. Mbinu**<br><br>Katika sura za makka imetumika lugha ya mchomo moja kwa moja kwa walengwa Mwenyezi Mungu ameapia maumbile mbalimbali ili yawe ushahidi uliowazi juu ya viumbe. | ambao wanapaswa kusimamishwa na kuendeleza Dola ya Kiislamu.<br><br>**2. Ujumbe**<br><br>Kwa kiasi kikubwa ulijihusisha na ujenzi wa jamii ya kiislamu usimamishaji, uendeshaji na ulinzi wa Dola ya kiislamu. Pia vippengele vya sheria na sera mbalimbali za maisha pamoaja na hukumu mbalimbali hubainishwa.<br><br>**3. Muundo**<br><br>Takriban sura ningi zimejengwa na aya ndefu zilizo na lugha ya kisheria inayofafanua masuala mbalimbali na kuyaweka bayana kiutekelezaji na nyingi ya sura ni ndefu.<br><br>**4. Mbinu**<br><br>Katika sura hizi imetumika lugha ya sheria au ufafanuzi ili kuwawezesha waumini kutekeleza uislamu vilivyo. Pia Mwenyezi Mungu ametumia historia ya mitume waliotangulia ili kuwakatisha tamaa wapinzani wa Dola ya kiislamu na kuwapa waumini moyo katika kupigania Dola ya kiislamu. |

**NB:** Utangulizi aeleze sura za Makka ni zipi na Madina ni zipi.
- Utangulizi = 1 ½
- Hoja 4 = @ 3 = 12
- Hitimisho = 1 ½

**Jumla 15**

13. Adam ni mtume wa mwanzo aliyeletwa na Allah (s.w), Adam ndiye alipewa elimu ya kila kitu hapa ulimwenguni. Kutokana na ubavu wa Adam alitoka Hawa. Yafuatayo ni mafunzo yatokanayo na historia ya Adam (a.s).
- Utukufu wa mtu katika uislamu hautokani nasaba, rangi, kabila ila uwajibikaji kwa Allah (s.w) unaolandana na elimu sahihi.
- Tujiepushe na tabia ya kiibilisi ya kumtukuza au kumdharau mtu kutokana na nasaba, rangi, sura hali yake ya kiuchumi nk.
- Tujiepushe na tabia ya kiibilisi ya kuwa na chuki binafsi dhidi ya watu wasio na hatia yoyote.
- Tujiepushe na tabia ya kiibilisi ya kibri na majivuno

- Tuwe na msimamo katika kutekeleza amri za Allah (s.w) na Mtume wake na tusiwe tayari kuyumbishwa na hadaa za shaitwani
- Tunapofikwa na tashwish za kishetani tujikinge kwa Allah (s.w)
- Muda wote waislamu hawana budi kuchukua tahadhari kwani kiasili uislamu ni dini yenye maadui miongoni mwa mashetani wa kijini na watu
- Mwanadamu tangu mwanzo wa kuumbwa kwake amekusudiwa kuwa khalifa katika ardhi na nyenzo kuu kumwezesha kuwa khalifa ni Elimu ya mazingira na mwongozo .

  - Utangulizi = 1 ½
  - Hoja 6 = @ = 12
  - Hitimisho = 1 ½

    **Jumla 15**